**Maswali na Majibu**

*1.* Neema ya Mungu ni nini?
*Ni upendo na ukarimu wa Mungu kuwapea Yesu ili awaokoe kama zawadi ya bure. Ni zawadi yenye hatustahili kupewa.*

*2.* Ni nini inatutenga na Mungu? *Dhambi.*

3. Nani anaweza kutuleta kwa Mungu? Anatuleta namna gani?
*Yesu. Kwa dhabihu ya uzima wake usio na mawaa kwa ajili yetu*.

*4.* Tunastahili kupata wokovu? *Hapana. Ni zawadi ya Mungu.*

*5.* Tunaweza kufuta mabaya yetu kwa kufanya mazuri mengi?
*Hapana. Dhambi zetu zinaweza kusamehewa na Mungu kwa neema.*

*6.* Tunaweza kusabuliwa kwamba tuko haki namna gani?
*Kwa kukubali zawadi ya Mungu ya neema, tukitubu na tusamehewe dhambi zetu na zifunikwe.*

7. Hatuwezi kupata wokovu kwa kufanya mazuri, kwa hivyo tunahitajika kufanya mazuri?
*Ndiyo. Tunatakiwa tuonyeshe shukrani kwa Mungu kwa kumpendeza*.

8. Mfano juu ya mfalme na mtumishi wake unatufundisha nini?
*Mungu ametuonyesha neema kubwa, nasi lazima tuonyeshe neema kwa wenzetu*.

9. Tunatakiwa tufanye nini ili tuwe tumekubali zawadi ya neema ya Mungu?
*Amini kwa Mungu, tubu, kuwa na imani, batizwa, samehewa, ishi maisha mapya ya kupendeza* Mungu.

*10.* Zawadi yetu itakuwa nini tukikubali neema ya Mungu?
*Maisha ya milele kwa Ufalme wa Mungu wakati Yesu atarudi hapa duniani.*

## Mistari ya kukariri

Zaburi 103:10 – 11; Zaburi 32:1 – 2; Warumi 6:1 – 2; Waefeso 2:8

## Mazungumzo

Zungumza juu ya maana ya neema ya Mungu na vile unaweza kuhesabiwa haki mbele ya Mungu. Zungumza vile unaweza kuonyesha neema kwa maisha yako.

## Kuandika

Andika hadithi yenye Yesu alisema juu ya mwana mpotefu. Mfano huu unatufunza somo gani kuhusu neema ya Mungu?

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 45 Neema ya Mungu

**SOMA Warumi 6:23; Luka 15:11 – 32; Zaburi 103:10 – 11; Isaya 59:2; Zaburi 32:1 – 2; Warumi 6:1 – 2; Waefeso 2:8; Mathayo 18:23 – 35**

**SOMO**

Kwa Biblia, neema ya Mungu ni upendo wake mzuri kwa watu. Si kitu chenye tunastahili kupata. Ni zawadi ya bure kutoka kwa Mungu. Mfano wa hii zawadi ni neema ya Mungu ya Bwana wetu Yesu Kristo kutuletea wokovu.

Kwa maisha yetu tumezoea kupata zawadi. Tunajifunza kufanya vizuri kwa michezo. Tunafanya kazi tupate mshahara. Tunasoma tupite mtihani. Zawadi ya neema ya Mungu ni tofauti kabisa. Biblia inatufunza kwamba hatustahili wokovu. Hatuwezi kufanya mambo mengi mazuri eti tupate nafasi kwa Ufalme wa Mungu. Kwa hali zote tunategemea neema ya Mungu.

Sote tumetenda dhambi kwa hivyo sote tutakufa. Mungu alituma Mwanawe wa pekee, Bwana Yesu Kristo, ulimwenguni ili atufungulie njia ya uzima. Dhambi zetu sinatutenga na Mungu. Yesu alikuja kurejesha watu kwa Mungu. Tukubali kwa unyenyekevu dhabihu ya Yesu ili tuwe na tumaini la uzima.

Watu wengi wanafikiri kwamba mazuri wanayofanya na mabaya, huwa yanaongezwa. Wakiwa na mazuri mengi kushinda mabaya, wanadhani wanakibali cha uzima wa Mungu. Hii si kweli. Ni rahisi kufikiri hivyo. Zawadi haipatikani hivyo. Ni mishahara ndiyo hupatikana namna hiyo. Paulo anatwambia, "Mshahara wa dhambi ni mauti; lakini karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu." (Warumi 6:23).

Yesu alipeana mfano wa mwana mpotefu. Mtu tajiri alikuwa na wana wawili. Mwana mkubwa alikuwa na akili na alifanya kazi kwa bidii. Mwana mdogo hakuwa mtulifu na alitaka kufanya vile alitaka. Aliuliza baba yake ampe fungu ya mali yake. Aliondoka, akaenda na kufanya vile alipenda. Aliharibu hiyo mali kwa matumizi yasiyofaa. Hatimaye aliishi kwa umasikini na njaa nyingi. Aliamua kwamba anaweza kuishi vizuri kwa baba yake lakini kama mtumwa. Alirudi nyumbani na kuomba msamaha kwa baba yake. Baba yake alimkaribisha nyumbani kama mwanawe kwa furaha kuu.

Hadithi ya mwana mpotefu inatufundisha juu ya upendo na huruma na neema ya Mungu. Baba kwa hiyo hadithi alionyesha upendo na huruma kwa mwanawe, hata kama alikuwa amekuwa na makosa. Baba yake hakumtendea vile makosa yake yalikuwa. Mungu atakuwa na huruma na atusamehe dhambi zetu hata kama hatustahili. Hii ni zawadi ya neema yake.

Dhambi inatutenga na Mungu kwa sababu Mungu hapendi dhambi. Tunatengwa na Mungu kama wenye dhambi. Mungu amepeana njia ya kufunika dhambi zetu ili tuwe na uhusiano Naye. Hakuna vile tunaweza kufunika dhambi zetu. Mungu alisema kwamba tunaweza kusamehewa dhambi kwa kutubu na kutoa dhabihu. Wakati wa Agano la Kale, wanyama walitolewa kama dhabihu. Yesu alipokuja aliishi maisha mazuri ya kutii Mungu. Hakutenda dhambi. Aliteswa na akafa msalabani. Yeye ndiye alikuwa dhabihu takatifu iliyotolewa kwa ajili ya dhambi zetu.

Hii ni zawadi ya neema ya Mungu kwetu. Ni nafasi yetu kuokoka kutoka dhambini. Kwa sababu ya Yesu kama dhabihu, dhambi zetu zinafunikwa na tunakuwa bila dhambi mbele ya Mungu. Hata kama sisi ni wachafu wa dhambi, kwa neema ya Mungu tunaweza kusamehewa na tuwe wasafi. Mungu anasema, "Hata kama dhambi zako ni nyekundu kama damu, nitazifanya nyeupe kama theluji." (Isaya 1:18).

Kama dhambi zetu zinafunikwa kwa dhabihu ya Yesu, Mungu hatusabulii dhambi tena. Anatusamehe dhambi zetu na tunahesabiwa wenye haki. Hata kama dhambi zetu ni mbaya namna gani, bado kwa neema ya Mungu zitafunikwa na kusamehewa tukitubu kwa kweli. Tukikubali neema ya Mungu, tunapata msamaha na kuweka dhambi mbali nasi. Tunaweza kuwa na amani na Mungu. Tunakuwa na uhusiano wa karibu na Mungu kama watoto Wake.

Tuwe tukikumbuka kwamba si kwa sababu ya mazuri tufanyayo au ufahamu wa Biblia itatuokoa. Hatutapata nafasi kwa Ufalme wa Mungu kwa sababu ya mazuri mengi tufanyayo. Hatuwezi kufuta mabaya tuliyofanya kwa kufanya mazuri. Mungu anataka tutubu dhambi zetu na tukubali neema na msamaha Wake.

Hatuwezi kupata wokovu kwa kufanya mazuri. Kwa hivyo hatustahili kufanya mazuri na hata kuishi kwa njia nzuri? Inamaanisha tuwache kufanya mazuri na tujifurahishe wenyewe? Paulo anazungumzia haya kwa barua yake kwa Warumi. "Tuendelee kufanya dhambi ndiyo neema iongezeke? La hasha" hatuwezi kufanya mazuri kupata wokovu. Tunatakiwa tushukuru Mungu kwa sababu ya kipawa chake kuu cha neema na tuishi kumpendeza.

Tunatakiwa tuonyeshe Mungu shukrani kwa jinzi tunavyoishi. Kila siku tuwe tukimshukuru kwa zawadi ya wokovu. Tuonyeshe wengine hiyo neema na tukue kwa hiyo neema. Tunaweza kufanya hivi ikiwa tutajaribu kuiga vile Yesu aliishi. Tuonyeshe neema kwa jinzi tunazungumza na watu na mienendo yetu iwe ya upendo.

Yesu alitwambia mfano wa vile mfalme alitaka kufanya hesabu na wafanyi kazi wake. Mfanyi kazi wa kwanza alidaiwa talanta 10,000 ya fedha. Hii ilikuwa pesa nyingi sana yenye huyo mtu hangeweza kulipa.
Mfalme aliamrisha kwamba yeye na familia yake wauzwe kama watumwa. Lakini vile yule mtu alimsihi aurumiwe, mfalme alimsamehe deni lote na kumwachilia aende. Yule mtumishi alitoka, na kule nje akakutana na mwenziwe aliyemdai senti 100. Mtu yule alimwomba amhurumie na mpe wakati ili alipe hilo deni. Lakini yule mtumishi wa kwanza alikataa na kumtupa gerezani. Mfalme aliposikia hayo, alikasirika sana. Alimwambia yule mtumishi kwamba, "Nilikuhurumia na nikakusamehe deni kubwa sana. Ungekuwa na huruma na umsamehe mwenzako hilo deni ndogo." Mfalme alimwadhibu yule mtumwa kwa sababu hakuonyesha huruma kwa mwenzake iliyoonyeshwa kwake.

Huu mfano unatufundisha kwamba Mungu amekuwa na huruma na neema kwetu. Tunastahili tuwe na shukrani kwa ajili ya neema Yake na tuonyeshe wenzetu vivyo hivyo.

Tumepewa zawadi ya neema ya Mungu bure. Ni wajibu kila mmoja wetu aamue mwenyewe kama anataka hiyo zawadi au la. Ikiwa tunakubali hiki kipawa cha Mungu, lazima tufanye yafwatayo:

- *Tuamini Mungu*
- *Tukumbuke kwamba sisi tu wenye dhambi*
- *Tutubu dhambi zetu*
- *Tuwe na imani kwamba tunaweza kuokolewa na Yesu.*
- *Tubatizwe.*
- *Tupate msamaha wa dhambi*
- *Tuishi maisha mapya na tumpendeze Mungu sio sisi wenyewe.*

Ni shukurani kuwa na neema ya Mungu inayotuwezesha tuwe na uamuzi wa kufuata Yesu. Tunajua kwamba hatuna nguvu wala uhaki wa kumpa Mungu. Ni neema yake inayotufundisha kukataa hii maisha yetu na kufuata Yesu Kristo kama wanafunzi wake. Ni neema yake inayotusaidie tumpendeze kwa hii maisha tunayoishi. Tukiwa na upendo na neema ya Mungu, tutapata nafasi kwa Ufalme wa Mungu.